JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2020

## KISWAHILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2020

# 021 KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO

YALIYOMO .......... iii
DIBAJI .......... iv
1.0 UTANGULIZI .......... 1
2.0 TATHMINI YA KILA SWALI .......... 2
2.1 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO .......... 2
2.1.1 Swali la 1: Ufahamu .......... 3
2.1.2 Swali la 2: Ufupisho .......... 9
2.2 SEHEMU B: SARUFI .......... 12
2.2.1 Swali la 3: Uundaji wa Maneno .......... 12
2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno .......... 15
2.3 SEHEMU C: MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA .......... 19
2.3.1 Swali la 5: Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali .......... 19
2.3.2 Swali la 6: Lugha ya Kimazungumzo .......... 23
2.4 SEHEMU D: FASIHI KWA UJUMLA .......... 26
2.4.1 Swali la 7: Fasihi Simulizi .......... 26
2.4.2 Swali la 8: Fasihi Simulizi .......... 29
2.4.3 Swali la 9: Fasihi Simulizi .......... 32
2.5 SEHEMU E: UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI .......... 36
2.5.1 Swali la 10: Uandishi .......... 36
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA .......... 39
4.0 HITIMISHO .......... 40
5.0 MAPENDEKEZO .......... 41
KIAMBATISHO A .......... 42
KIAMBATISHO B .......... 43

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali na viwango vya ufaulu vya wanafunzi katika Upimaji wa Kidato cha Pili mwaka 2020 kwa somo la Kiswahili. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali katika upimaji huu. Majibu ya wanafunzi ni ishara inayoonesha mafanikio chanya au hasi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza na cha Pili. Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu unathibitisha mambo waliyoweza kujifunza kwa ufanisi na yale walioshindwa.

Taarifa hii imechambua sababu zilizochangia wanafunzi kujibu maswali kwa usahihi au kushindwa kujibu kulingana na matakwa ya swali. Matokeo ya uchambuzi huu yamebainisha baadhi ya sababu zilizowafanya kupata alama za juu kama vile kuelewa matakwa ya swali, kuwa na maarifa/ujuzi katika kuelezea dhana mbalimbali na kuwa na uelewa wa mada zilizopimwa. Aidha, sababu za wanafunzi kupata alama hafifu zimechangiwa na kukosa maarifa/ujuzi wa kutosha kuhusu mada mbalimbali za somo la Kiswahili, kushindwa kutumia kanuni sahihi za lugha pamoja na kutokuelewa matakwa ya swali ipasavyo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho huu utawawezesha wadau wa elimu, walimu na wanafunzi kutafuta mbinu za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji ili kutatua kasoro mbalimbali zilizobainishwa katika taarifa hii. Aidha, ni matarajio ya Baraza kuwa, maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi ipasavyo, wanafunzi wa Kidato cha Pili wataweza kutumia kanuni sahihi za lugha na kufafanua dhana mbalimbali kwa ufasaha.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukurani kwa Maafisa Mitihani, walimu, wadau wengine wa elimu na wengine wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kidato cha Pili ulifanyika mwezi Novemba mwaka 2020. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu umezingatia kikamilifu muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Kidato cha I na II. Aidha, upimaji huo ulikuwa na maswali 10 yaliyogawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za *Ufahamu*, *Sarufi*, *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha*, *Fasihi* na *Uandishi* mtawalia. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu zote.

Upimaji wa somo la Kiswahili ulifanywa na jumla ya wanafunzi 601,458 kati ya wanafunzi 646,195 walioandikishwa mwaka 2020. Miongoni mwao, wavulana walikuwa 277,647 na wasichana 323,811.

Taarifa hii inachambua viwango vya ufaulu wa wanafunzi wa Kidato cha Pili katika Upimaji wa somo la Kiswahili kwa mwaka 2020. Jumla ya wanafunzi 555,232 sawa na asilimia 92.38 walifaulu kwa kupata daraja A hadi D. Kiwango hicho cha ufaulu ni cha juu kwa ongezeko la asilimia 0.19 ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo asilimia 92.19 ya wanafunzi ndio waliofaulu. Ufaulu wa wanafunzi kwa kila daraja umeoneshwa katika **Jedwali Na. 1**.

| **Mwaka** | **Waliofanya** | **Madaraja** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **A** | **B** | **C** | **D** | **F** |
| 2019 | 571,116 | 27,448 | 70,766 | 270,797 | 157,089 | 44,571 |
| 2020 | 601,458 | 52,116 | 110,663 | 266,161 | 126,292 | 45,771 |

**Jedwali Na. 1**: Ufaulu wa Wanafunzi kwa kila Daraja kwa Mwaka 2019 na 2020

Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni kiwango *kizuri, wastani* na *hafifu*. Kiwango kizuri cha ufaulu kimeanzia alama 65 hadi 100, kiwango cha wastani kikianzia alama 30 hadi 64 na kiwango hafifu alama 0 hadi 29. Aidha, chati mbalimbali zimetumika ili kufafanua viwango hivyo ambapo rangi ya kijani inawakilisha kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha kiwango cha wastani na rangi nyekundu ikiwakilisha kiwango

hafifu cha ufaulu. Hata hivyo, sampuli za majibu ya wanafunzi zimeambatanishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kile kilichofanywa na wanafunzi.

Kwa jumla, uchambuzi huu unalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika mkakati wa kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kwa vizazi vijavyo.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Sehemu hii inafafanua kwa kina uchambuzi wa kila swali na majibu yaliyotolewa na wanafunzi kwa kuonesha maswali yaliyojibiwa vizuri na yale yaliyojibiwa vibaya. Aidha, sababu za ufaulu wa viwango mbalimbali zimeelezwa bayana kwa kila swali. Sambamba na hayo, sampuli za majibu ya wanafunzi kwa kila swali zimeambatanishwa ili kuthibitisha maelezo yaliyotolewa katika uchambuzi huu.

## 2.1 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili yaliyomtaka mwanafunzi kuonesha umahiri katika kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali kisha kufupisha habari hiyo. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa:

> *Jambo moja kubwa katika mambo ya huzuni kwa watu wote sasa lilitokea. Mke wangu mpenzi alishikwa na maradhi, na baada ya muda kidogo wa udhaifu na maumivu akafariki dunia. Utengano huu kati yetu ulitokea baada ya miaka kumi ya kuishi pamoja kwa mapenzi, amani, raha na baraka. Tukio hili lilikuwa pigo kubwa sana kwangu na msiba mkubwa katika nyumba nzima. Marehemu huyu alikuwa* ***tunu*** *ya maisha yangu, tegemeo na mshauri mwema. Alinisaidia katika mambo mengi wakati wa maisha yetu pamoja ambayo yangalinishinda kuyatenda mimi peke yangu.*
>
> *Sura yake ilikuwa jamali kwa* ***kimo cha kadiri****, uso ulikuwa mviringo wa yai, nywele nyeusi za kushuka, paji pana, nyusi za upindi, macho mazuri yalikuwa na tazamo juu ya kila kitu, kope za kutana, masikio ya kingo yasiyopitwa na sauti ndogo, meno ya mwanya yaliyojipanga vizuri mithili ya lulu katika chaza, ulimi wa fasaha na maneno ya kiada yaliyotawaliwa, midomo imara isiyokwisha tabasamu. Sauti pole na tamu kama wimbo, kidevu cha mfuto katikati yake palikuwa na*

*kidimbwi kidogo. Shingo kama mnara ambayo juu yake paliota kichwa cha mawazo mengi, chini ya shingo mabega yalikuwa kama matawi ya maua, kifua cha madaha, mikono ya mbinu, tumbo jembamba na miguu ya mvungu. Uzuri wake ulikuwa kamili. Kwa tabia alikuwa mwaminifu na mfano wa kuiga katika nyumba.*


*Wanawake ni wengi kama walivyo wanaume lakini wenye sura kama iliyoelezwa ni* ***adimu*** *sana kukutana nao duniani. Kabla ya kuoa nililitafuta umbo namna yake muda wa miaka kumi. Kitu nilichokuwa nakitafuta kwa muda wote mwisho nilikipata, lakini baada ya miaka kumi mingine kilikwenda* ***safari ya watu wasikorudi*** *na wito usiofika. Mauti yake ya mapema yalikuwa ni msiba na hasara kubwa sana kwangu. Nilishindwa kujizuia kama nilivyotaka, machozi yalinitoka mengi sana na yalikuwa hayazuiliki sababu ya pigo zito lililonijia.*

### 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu* ambapo mwanafunzi alitakiwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyofuata. Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kutumia maarifa ili kujibu maswali yaliyotokana na kusoma kifungu cha habari. Swali lilikuwa na jumla ya alama 9 na liligawanyika katika vipengele vinne yaani (a) hadi (d).

Kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi aandike kichwa cha habari kwa maneno yasiyozidi matano kutokana na habari aliyosoma, (b) (i) kilimtaka mwanafunzi ataje jambo linaloleta huzuni kwa watu wote kama lilivyomtokea mwandishi wa habari aliyosoma, (b) (ii) kilimtaka mwanafunzi kubainisha muda ambao mwandishi wa habari aliyosoma aliishi na mkewe baada ya harusi yao. Aidha, katika kipengele (c) (i) mwanafunzi alitakiwa kueleza tabia ya mke wa mwandishi wa habari, kipengele (c) (ii) kilimtaka aeleze maana ya usemi wa mwandishi "uzuri wake ulikuwa kamili" kutoka katika aya ya pili ya habari na kipengele (d) (i) hadi (iv) kilimtaka mwanafunzi aandike maana ya maneno au vifungu vya maneno kama vilivyotumika katika habari aliyosoma.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 601,475 sawa na asilimia 100 ambapo asilimia 91.3 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 1***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 41.8 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 9. Kwa upande mwingine, asilimia 49.5 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 5.5 na asilimia 8.7 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5.

Asilimia 49.5 ya wanafunzi waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza katika baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alimudu kutoa majibu sahihi katika vipengele (a) hadi (c) lakini katika kipengele (d) alishindwa kueleza maana za maneno/vifungu vya maneno katika vipengele vyote ambapo aliandika: (i) Tunu - *ahadi*, (ii) Kimo cha kadiri - *weupe wa asili*, (iii) Adimu - *nzuri*, na (iv) Safari ya watu wasikorudi - *Marekani*; maana ambazo hakumaanisha mwandishi wa habari husika. Majibu sahihi katika kipengele (d) ni kama ifuatavyo: (i) Tunu - zawadi ya pekee, (ii) Kimo cha kadiri - urefu wa wastani, (iii) Adimu - haba/siopatikana kwa urahisi na (iv) Safari ya watu wasikorudi kuwa - ahera/kufa.

Wanafunzi wengine (41.8%) walipata alama za juu kwa kuwa waliweza kujibu vipengele vingi kwa usahihi kutokana na kuelewa

vizuri kifungu cha habari walichokisoma. Wanafunzi hao, katika kipengele (a) waliandika kwa usahihi kichwa cha habari kwa maneno yasiyozidi matano na kwa herufi kubwa kama *MSIBA WA MKE WANGU/KIFO CHA MKE WANGU.* Aidha, katika kipengele (b)(i) waliweza kutaja *kifo/kufiwa* kama jambo kubwa liletalo huzuni kwa watu wote kama lililomtokea mwandishi wa habari hiyo na katika kipengele cha (b) (ii) walibaini kwa usahihi muda sahihi ambao mwandishi wa habari husika aliishi na mke wake baada ya harusi yao kuwa ni *miaka kumi*. Katika kipengele (c) (i) waliweza kueleza tabia ya mke wa mwandishi wa habari husika kuwa alikuwa *mwaminifu na mfano wa kuiga katika nyumba* na (c) (ii) waliweza kueleza alichomaanisha mwandishi kuhusu uzuri wa mke wake kukamilika yaani *hakuwa na kasoro*. Pia, katika kipengele (d) waliweza kuandika maana ya maneno au vifungu vya maneno vilivyotumika katika habari husika kama ifuatavyo: (i) Tunu ni *zawadi ya pekee*, (ii) Kimo cha kadiri ni *urefu wa wastani*, (iii) Adimu ni *haba/siopatikana kwa urahisi* na (iv) Safari ya watu wasikorudi kuwa ni *ahera/kufa*. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari uliyosoma kwa maneno yasiyozidi matano.

MSIBA WA MKE WANGU

(b) (i) Ni jambo gani kubwa liletalo huzuni kwa watu wote lililomtokea mwandishi wa habari hii?

Kifo cha mke wake aliyempenda sana.

(ii) Ni muda gani mwandishi wa habari hii aliishi na mkewe baada ya harusi yao?

Waliishi miaka kumi.

(c) (i) Mke wa mwandishi wa habari hii alikuwa na tabia ya namna gani?

Alikuwa mwaminifu na mfano wa kuiga katika nyumba.

(ii) Katika aya ya pili mwandishi ana maana gani anaposema uzuri wake ulikuwa kamili?

Mwandishi anamaanisha kwamba uzuri wa mke wake ulikua ume-kamilika yaani hana kasoro.

(d) Andika maana ya maneno au vifungu vya maneno kama vilivyotumika katika habari uliyosoma:

(i) Tunu… Zawadi ya pekee.

(ii) Kimo cha kadiri… Urefu wa wastani.

(iii) Adimu… Kisichopatikana kwa urahisi.


(iv) Safari ya watu wasikorudi… Amekufa.

Kielelezo Na. 1.1: *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.*

Katika Kielelezo Na. 1.1, mwanafunzi alijibu vipengele vyote kwa usahihi kwa kuandika kichwa cha habari kwa idadi sahihi ya maneno, kutaja jambo kubwa liletalo huzuni kwa watu wote lililomtokea mwandishi wa habari husika, kubaini muda ambao mwandishi wa habari hiyo aliishi na mkewe baada ya harusi yao, kueleza tabia ya mke wa mwandishi wa habari hiyo, kutoa maana ya uzuri kamili wa mke wa mwandishi na kueleza kinagaubaga maana ya maneno au vifungu vya maneno vilivyotumika katika habari hiyo.

Aidha, wanafunzi wachache (8.7%) walishindwa kujibu vipengele vingi vya swali hili na kupata alama hafifu. Baadhi yao, hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuelewa kifungu cha habari walichokisoma hivyo kushindwa kutoa majibu sahihi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipengele (a) alitoa maelezo kuhusu kichwa cha habari kwa kuandika, "*Kichwa cha habari huandikwa kwa herufi kubwa*" badala ya kuandika kichwa stahiki cha habari aliyopewa yaani *MSIBA WA MKE WANGU/KIFO CHA MKE WANGU*. Katika kipengele (b) (i) mwanafunzi huyo alishindwa kubainisha jambo lileltalo huzuni kwa watu wote ambalo ni *kifo* kama lilivyomtokea mwandishi wa habari aliyosoma, badala yake aliandika kuhusu mke wa mwandishi kushikwa na maradhi kinyume na matakwa ya swali.

Vilevile, katika kipengele (c) (i) alishindwa kueleza tabia ya mke wa mwandishi wa habari hiyo kama mtu *mwaminifu na mfano wa kuiga katika nyumba yao* badala yake alielezea wasifu wa mke wa mwandishi na katika (c) (ii) alishindwa kueleza maana ya usemi wa mwandishi kuwa uzuri wa mke wake ulikuwa kamili yaani *bila kasoro* badala yake alieleza tabia ya mke wa mwandishi. Vivyo hivyo, katika kipengele (d) alishindwa kuandika maana ya maneno/vifungu vya maneno kama yalivyotumika katika habari badala yake alidondoa baadhi ya maneno na vifungu vya maneno vilivyotumika katika habari visivyokuwa na uhusiano na maneno/vifungu vya maneno alivyopewa. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali na kupata alama hafifu.



**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari uliyosoma kwa maneno yasiyozidi matano.

Kichwa cha habari kinasema tufatilie sheria za watu wa kubwa Mfano wazee na tuifatilie Mambo ya Mababa.

(b) (i) Ni jambo gani kubwa liletalo huzuni kwa watu wote lililomtokea mwandishi wa habari hii?

Mkewangu Mpenzi alishikwa na Maradhi

(ii) Ni muda gani mwandishi wa habari hii aliishi na mkewe baada ya harusi yao?

utengano huu kafi kefu ulitokea baada ya Miaka 10 Yakuishi pamoja kwa Mapenzi, ata amani na baraka

(c) (i) Mke wa mwandishi wa habari hii alikuwa na tabia ya namna gani?

tabia ya sura yake ilikuwa jamali kwa kimo cha kadiri uso ulikuwa Mviringo wa yai Nywele nyeusi za kuhuka, paji pana nyusi za upindi, Macho Mazuri Yalikuwa na Mtazamo ya kila kitu hiyo ndo tabia yake kubadilisha sura.

(ii) Katika aya ya pili mwandishi ana maana gani anaposema uzuri wake ulikuwa kamili?

kwa tabia alikuwa Mwaminifu na Mfano wa kuiga katika nyumba.

(d) Andika maana ya maneno au vifungu vya maneno kama vilivyotumika katika habari uliyosoma:

(i) Tunu……Kami Maisha yangu, tegemeo na Mhami Mwema

(ii) Kimo cha kadiri……Ni uso ulikokuwa na Mviringo wa yai nywele nyeusi za kuhuka, paji pana, nyusi za upindi Macho Mazuri Yaliyo kuwa na Mtazamo.

(iii) Adimu……ni Wanawake wengi kama walivyo wanaume lakini wenye sura kama iliyoelezwa


(iv) Safari ya watu wasikorudi……ni wito wa fika au ni kitu alicho kuwa anakitafuta kwa Mda wote Mwisho alikipata baada ya Miaka 10

Kielelezo Na. 1.2: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 1.*

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu vipengele (a), (b) (i), (c) na (d) hivyo kupata alama hafifu. Hata hivyo, mwanafunzi huyo katika kipengele (b) (ii) aliweza kubaini muda wa *miaka kumi* ambao mwandishi wa habari husika aliishi na mkewe baada ya harusi yao.

### 2.1.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutumia maarifa ili kufupisha habari aliyoisoma. Swali lilikuwa na jumla ya alama 6 na lilimtaka mwanafunzi kufupisha habari kwa maneno sitini (60). Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na wanafunzi wengi (596,657) sawa na asilimia 99.2 ya waliofanya upimaji huu. Kiwango cha ufaulu kinaonesha kuwa asilimia 86.6 ya wanafunzi waliopimwa walifaulu kuanzia kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2.*

Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa wanafunzi ambapo asilimia 31.9 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 4 hadi 6, asilimia 54.7 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 3.5 na asilimia 13.4 walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 hadi 1.5.

Asilimia 54.7 ya wanafunzi waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kuandika ufupisho usiojitosheleza. Aidha, wanafunzi hao walishindwa kuzingatia baadhi ya mambo muhimu ya kufupisha habari kama vile; kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha maana iliyoko katika habari, kuwa na mtiririko wenye mantiki, kuzingatia wazo kuu la habari na idadi ya maneno yasiyopungua sitini (60). Wanafunzi hao waliweza kuzingatia baadhi ya vigezo hivyo kwa usahihi na vingine vikiachwa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika ufupisho wenye kuzingatia

baadhi ya vigezo lakini alitumia maneno pungufu ya sitini (60) hivyo kupata alama za wastani.

Vilevile, asilimia 31.9 ya wanafunzi walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu. Baadhi yao, waliandika ufupisho uliokuwa na dosari ndogo ndogo za kitahajia, kimtiririko na kimsamiati. Wanafunzi wengine, (2,052) sawa na asilimia 0.3 walipata alama zote (6) kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika kufupisha habari kama vile; kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha kiini cha habari, kubaini mawazo makuu, kupanga kazi katika mtiririko unaoleta mantiki na kuzingatia idadi ya maneno. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyefupisha habari kwa kuzingatia mambo muhimu na kupata alama za juu.

2. Andika ufupisho wa habari uliyosoma kwa maneno sitini (60).

Huzuni kubwa ilinifika pale nilipofiwa na mke wangu kipenzi. Marehemu huyu alikuwa ni mtu wa pekee sana kwangu, kwani alinisaidia kwenye mambo magumu yaliyonishinda. Licha ya hivyo hakuna wa kufanana naye kwani alikuwa mrembo, mwenye tabasamu lisilokwisha na mwaminifu siku zote. Ni bahati sana katika jamii kuwa na watu kama hawa. Hii ndiyo maana ilinuwia vigumu sana kuvumilia majonzi haya.

Kielelezo Na. 2.1: *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 2.*

Katika Kielelezo Na. 2.1, mwanafunzi alifupisha habari kwa kuzingatia mawazo makuu, kupanga kazi katika mtiririko unaoleta mantiki, idadi stahiki ya maneno na kutumia maneno yake mwenyewe bila kupotosha kiini cha habari.

Hata hivyo, asilimia 13.4 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama hafifu kutokana na kuandika ufupisho usiokidhi vigezo stahiki. Baadhi yao, walitumia maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari, kutokuzingatia idadi ya maneno, mpangilio wenye kuleta mantiki na kushindwa kubaini mawazo makuu katika habari waliyopewa, hivyo kupata alama za chini. Aidha, wanafunzi wengine (29,357) sawa na asilimia 4.9 waliandika ufupisho usiozingatia vigezo vyote na kupata 0. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika ufupisho

wenye *maneno (171)* badala ya sitini (60), alitumia maneno kama yalivyo kwenye habari aliyopewa badala ya kutumia maneno yake mwenyewe na *kutokuzingatia mpangilio wenye mantiki* na kupata alama za chini. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyefupisha habari bila kuzingatia taratibu za uandishi wa ufupisho na kupata alama hafifu.

2. Andika ufupisho wa habari uliyosoma kwa maneno sitini (60).

jambo moja kubwa katika mambo ya uzuni kwa watu
wote. Mke wangu alishikwa na Maradhi na Udhaifu
akafariki dunia. Utengano huu kati yetu ulitokea kati
ya Miaka kumi ya kuishi pamoja kwa Mapenzi
Tukio hili lilikua kubwa Sana kwangu na msiba
mkubwa katika nyumba nzima. Marehemu alikua tunu ya
Maisha yangu.

Sura yake ilikuwa hamali kwa kimo cha kadri uso ulikuwa
muiringo wa yai nywele nyeusi, paji pana nyusi za upinde
kope za kutona, masikio ya kingo sauti ndogo, Meno ya Mwanya.
Ulimi wa fasaha na Maneno ya ~~kitaka~~ kida midomo isiyo
kwisha tabasamu kichwa cha Mawazo mengi / kifuko cha mada
ha, tumbo jembamba na miguu ya mivungu uzuli wake ulika
wa kamili. Matabia alikuwa Mwaminifu na Mpono wa kuig
a katika nyumba.

Wanawake ni wengi kama Wanaume wenyesura kama aliye elezwa adim
kabla ya kuwa nilitafuta umbo namna yake ndani ya miaka kumi
mengine ikalikwanda. Safari ya Watu wasikorudi. Mauti yake
ni msiba na hasara kubw. Sana kwangu. Nilishindwa kuzuia
kama nilivyotaka. Machozi yalinitoka mengi sana yalikuwa ayazuilika
Sababu ya pigo mito lililonijia.

Kielelezo Na. 2.2: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 2.*

Katika Kielelezo Na. 2.2, mwanafunzi alinakili habari aliyopewa bila kutumia maneno yake mwenyewe na kutumia idadi kubwa ya maneno kinyume cha matakwa ya swali.


## 2.2 SEHEMU B: SARUFI

Sehemu hii ilihusu Sarufi na ilikuwa na maswali mawili yaliyomtaka mwanafunzi kuonesha umahiri wa kunyambua, kuunda na kubainisha maneno mbalimbali.

### 2.2.1 Swali la 3: Uundaji wa Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* hususan mada ndogo ya *Kutumia Mnyumbuliko.* Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kuunda maneno ya Kiswahili na lilikuwa na jumla ya alama 10. Swali lilikuwa na vipengele viwili ambapo kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi kunyambua maneno (i) Toa, (ii) Fyeka, (iii) Ondoa, (iv) Piga na (v) Lia kwa kutumia kauli ya kutendeana. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kuunda nomino moja kwa kila kipengele kutokana na vitenzi (i) Lea, (ii) Nyoa, (iii) Pika, (iv) Cheza na (v) Soma.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 600,667 sawa na asilimia 99.9 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani asilimia 53.3 walifaulu kwa kupata alama za wastani hadi za juu. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.





**Chati Na. 3***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3.*

Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 18.8 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10, asilimia 34.5 walifaulu kwa kiwango cha

wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na asilimia 46.7 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Kati ya wanafunzi waliojibu vizuri swali hili, asilimia 34.5 walipata alama za wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza katika baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliweza kunyambua maneno katika vipengele vitatu yaani (a) (i), (iii) na (iv) lakini alishindwa kunyambua maneno katika vipengele (ii) *Fyeka* na (v) *Lia* kwa kuandika *fyekana* na *limiana* mtawalia badala ya kuandika (ii) Fyekeana na (v) Liliana. Hata hivyo, mwanafunzi huyo alijibu kwa usahihi kipengele (b) na kupata alama za wastani.

Aidha, wanafunzi wachache (18.8%) ndio waliojibu vizuri na kupata alama za juu kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mnyumbuliko wa vitenzi kwa kutumia kauli ya kutendeana na uundaji wa nomino. Wanafunzi hao, waliweza kunyumbua maneno kwa kutumia kauli ya kutendeana yenye maumbo –e-an- na –i-an- katika vipengele (a) kama ifuatavyo: (i) Toa - *Toleana*, (ii) Fyeka - *Fyekeana*, (iii) Ondoa - *Ondoleana*, (iv) Piga - *Pigiana* na (v) Lia - *Liliana*. Aidha, katika kipengele (b) waliweza kuunda nomino moja kwa kila kitenzi walichopewa kama vile; (i) Lea - *Mlezi/malezi/mleaji*, (ii) Nyoa - *Kinyozi/ mnyoaji*, (iii) Pika - *Mpishi/mapishi/Mpikaji*, (iv) Cheza - *Mchezo/mchezaji* na (v) Soma - *Somo/msomaji/msomi*. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu vizuri swali hili na kukidhi matakwa ya swali katika vipengele (a) na (b) na kupata alama zote 10 za swali hili. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi huyo.


3. (a) Nyambua maneno yafuatayo kwa kutumia kauli ya kutendeana.

(i) Toa ........toleana..........

(ii) Fyeka .....fyekeana..........

(iii) Ondoa .....ondoleana..........

(iv) Piga ........pigiana..........

(v) Lia ...........liliana..........

(b) Unda nomino moja tu kutokana na vitenzi vifuatavyo:

(i) Lea .....mlezi..........

(ii) Nyoa ....kinyozi..........

(iii) Pika ......mpishi..........

(iv) Cheza ....mchezo..........

(v) Soma .....msomi..........


**Kielelezo Na. 3.1**: *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 3.*

Katika Kielelezo Na. 3.1, mwanafunzi alinyumbua maneno yote kwa kutumia kauli ya kutendeana na kuunda nomino stahiki kutokana na vitenzi alivyopewa kwa usahihi.

Licha ya swali hilo kuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, asilimia 46.7 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama hafifu kutokana na kushindwa kujibu vipengele vingi kwa usahihi. Kati yao, asilimia 26.1 walishindwa kujibu vipengele vyote na kupata 0. Wanafunzi hao, walionesha kukosa uelewa juu ya *unyambuaji wa maneno* kwa kutumia kauli ya kutendeana na *uundaji wa nomino* unaotokana na vitenzi. Baadhi yao, katika kipengele (a) walinyambua maneno waliyopewa kwa kutumia kauli ya kutendana yenye umbo la (-an-) kama vile; (i) Toa - *Toana*, (ii) Fyeka - *Fyekana*, (iii) Ondoa - *Ondoana* (iv) Piga - *Pigana* na (v) Lia - *Liana*. Wengine, walibainisha kimakosa viambishi katika maneno hayo yaani viambishi awali, mzizi na tamati kwa kuandika; (i) Toa - (*to -) kiambishi mzizi* na *(-a) kiambishi tamati*. Hali kadhalika, wengine walitunga sentensi zenye ujumbe mbalimbali kwa kutumia maneno katika kipengele (a) (i) hadi (v) badala ya kunyambua maneno hayo kwa kutumia kauli ya kutendeana yenye maumbo (-i-an-) na (-e-an-) kama vile; (i) Toleana, (ii) Fyekeana (iii) Ondoleana, (iv) Pigiana na (v) Liliana.

Katika kipengele (b), baadhi ya wanafunzi hawakuwa na ujuzi wa kunominisha vitenzi, badala yake walinyumbua vitenzi hivyo kwa kutumia kauli mbalimbali, kutunga sentensi kwa kutumia vitenzi (b)

(i) hadi (v) na wengine waliandika nomino ambazo haziendani na vitenzi walivyopewa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliunda nomino elekezi kwa vitenzi alivyopewa kama ifuatavyo: (i) Lea - *Mtoto* (ii) Nyoa - *Nyoka*, (iii) Pika - *Boga*, (iv) cheza - *Mpira* na (v) Soma - *Kitabu*. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata 0.


3. (a) Nyambua maneno yafuatayo kwa kutumia kauli ya kutendeana.

(i) Toa ...Toana...

(ii) Fyeka ...Fyekaana...

(iii) Ondoa ...Ondoana...

(iv) Piga ...Pigaana...

(v) Lia ...Liana...

(b) Unda nomino moja tu kutokana na vitenzi vifuatavyo:

(i) Lea ...Mama leo ameLiLi na zawaidi...

(ii) Nyoa ...Juma ananyoa ndevu zake...

(iii) Pika ...Dada anapika pilau...

(iv) Cheza ...Asha anacheza mpira wa miguu.

(v) Soma ...Omary anasoma kitabu...

Kielelezo Na. 3.2*: Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 3.*

Katika Kielelezo Na. 3.2, mwanafunzi alinyambua maneno katika kipengele (a) (i) hadi (v) kwa kutumia kauli ya kutendana (-an-) badala ya kutendeana (-e-an-) na (-i-an-) na katika kipengele (b) alitunga sentensi kwa kutumia vitenzi (b) (i) hadi (v) badala ya kuunda nomino kutokana na vitenzi hivyo kama ilivyotarajiwa.

### 2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno*, mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Aina za Maneno*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuchambua na lilikuwa na jumla ya alama 10. Swali hili lilikuwa na vipengele kumi vilivyomtaka mwanafunzi kubainisha nomino dhahania katika sentensi (a) hadi (j).

Wanafunzi 597,802 sawa na asilimia 99.4 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji walijibu swali hili na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu ambapo asilimia

71.3 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.

**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi**

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.5 | 171,596 | 28.7 |
| 3.0 - 6.0 | 139,886 | 23.4 |
| 6.5 - 10 | 289,347 | 47.9 |

Wanafunzi (289,347) sawa na asilimia 47.9 walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu. Wanafunzi hao, walikuwa mahiri katika kuchambua aina za maneno hivyo kuweza kubainisha nomino dhahania katika sentensi walizopewa. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyebainisha nomino dhahania katika sentensi zote alizopewa kwa usahihi na kupata alama zote za swali hili.

4. Bainisha nomino dhahania katika sentensi zifuatazo:

(a) Ugonjwa uliotokea uliua watu wengi.
Ugonjwa

(b) Shibe hulevya watu na wanyama.
Shibe

(c) Mwanadamu huangamia kwa kukosa maarifa.
Maarifa

(d) Timu ya kijiji ilipata ushindi katika mechi ya jana.
Ushindi

(e) Jumbe alishindwa mtihani kwa sababu ya starehe.
Starehe

(f) Gauni alilovaa limempendeza sana lakini uzuri nao unachangia.
Uzuri

(g) Uvivu ni janga la taifa.
Uvivu

(h) Ukosefu wa mvua husababisha njaa.
Njaa

(i) Anasa huzorotesha maendeleo.
Anasa

(j) Mwanafunzi anapofaulu mtihani huwa na furaha kubwa.
Furaha

Kielelezo 4.1*: Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 4.*

Katika Kielelezo Na. 4.1 mwanafunzi alibainisha kwa usahihi nomino dhahania katika sentensi (a) hadi (j) kwa kuzingatia matakwa ya swali.

Aidha, asilimia 23.4 ya wanafunzi waliojibu swali hili waliweza kubainisha nomino dhahania kwa baadhi ya sentensi na kushindwa katika sentensi nyingine hivyo kupata alama za wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele.

Hata hivyo, wanafunzi 171,596 sawa na asilimia 28.7 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5 kutokana na kushindwa kubainisha nomino dhahania katika sentensi walizopewa. Aidha, wanafunzi hao walikosa maarifa stahiki kuhusu aina za nomino katika muundo wa sentensi (a) hadi (j). Miongoni mwao, asilimia 14.7 walipata 0 kutokana na kushindwa kubaini neno hata moja ambalo ni nomino dhahania. Baadhi ya wanafunzi walibaini majina mengine yaliyotumika katika sentensi hizo yasiyo na sifa ya dhahania kwa kuandika (a) *watu* badala ya ugonjwa , (b) wanyama - badala ya *shibe*, (c) mwanadamu badala ya *maarifa*, (d) timu/mechi/jana badala ya *ushindi*, (e) Jumbe badala ya *starehe*, (f) gauni badala ya *uzuri*, (g) janga/taifa badala ya *uvivu*, (h) mvua badala ya *njaa*, (i) maendeleo badala ya *anasa* na (j) mwanafunzi badala ya *furaha* kama ilivyotakiwa. Wanafunzi wengine walibaini vitenzi kinyume cha matakwa ya swali na kupata 0 kama Kielelezo Na. 4.2 kinavyodhihirisha sampuli ya majibu ya mwanafunzi huyo.

4. Bainisha nomino dhahania katika sentensi zifuatazo:

(a) Ugonjwa uliotokea uliua watu wengi.

......uliotokea ni nomino dhahania......

..............................................................

(b) Shibe hulevya watu na wanyama.

......hulevya ni nomino dhahania......

..............................................................

(c) Mwanadamu huangamia kwa kukosa maarifa.

......huangamia ni nomino dhahania......

..............................................................

(d) Timu ya kijiji ilipata ushindi katika mechi ya jana.

......ilipata ni nomino dhahania......

..............................................................

(e) Jumbe alishindwa mtihani kwa sababu ya starehe.

......alishindwa ni nomino dhahania......

(f) Gauni alilovaa limempendeza sana lakini uzuri nao unachangia.

......Limempendeza ni nomino dhahania......

..............................................................

(g) Uvivu ni janga la taifa.

......Janga ni nomino dhahania......

..............................................................

(i) Anasa huzorotesha maendeleo.

......huzorotesha ni nomino dhahania......

..............................................................

(j) Mwanafunzi anapofaulu mtihani huwa na furaha kubwa.

......anapofaulu ni nomino dhahania......

Kielelezo Na. 4.2: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 4.*

Katika Kielelezo Na. 4.2, mwanafunzi alishindwa kubainisha nomino dhahania katika sentensi alizopewa badala yake alibainisha vitenzi vilivyotumika kwenye sentensi alizopewa katika kipengele (a) hadi (j).


## 2.3 SEHEMU C: MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili yaliyomtaka mwanafunzi kuonesha uwezo wa kutumia lugha katika miktadha mbalimbali na katika mawasiliano.

### 2.3.1 Swali la 5: Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali

Swali lilitoka katika mada *ya Mawasiliano*, mada ndogo ya *Lugha kama Chombo cha Mawasiliano*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuelewa dhana mbalimbali za lugha na lilimtaka kueleza maana ya istilahi zifuatazo: (a) Mawasiliano, (b) Silabi (c) Lugha, (d) Irabu na (e) Sentensi, kisha kutoa mfano kwa kila istilahi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi (600,381) sawa na asilimia 99.8 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa kiwango cha juu ambapo asilimia 90.6 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 4:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 5.*

Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 29.4 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10, asilimia 61.2 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na asilimia 9.4 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5.

Asilimia 61.2 ya wanafunzi waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kueleza maana ya baadhi ya istilahi kwa usahihi na kushindwa katika istilahi nyingine. Baadhi yao, waliweza kueleza maana ya istilahi lakini walishindwa kutoa mfano mahsusi kwa baadhi ya istilahi na kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi wengine sawa na asilimia 29.4 walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu kwa kuwa waliweza kueleza kwa usahihi maana ya istilahi walizopewa na kutoa mfano kwa kila istilahi. Wanafunzi hao walionesha uelewa wa hali ya juu kuhusu dhana mbalimbali zinazotumika katika mawasiliano kwa ujumla, hivyo kumudu kufasili istilahi kama ifuatavyo; (a) Mawasiliano kama *upashanaji wa habari*, (b) Silabi - *muunganiko wa konsonanti na irabu ambao hutamkwa kama fungu moja la sauti* (c) Lugha - *Sauti za nasibu zilizokubaliwa na jamii kutumika katika mawasiliano,* (d) Irabu - *herufi zinazotamkwa bila kizuizi* na (e) Sentensi - *tungo iliyojitosheleza kimaana*. Pia, wanafunzi hao waliweza kutoa mifano sahihi inayofungamana na istilahi hizo na kupata alama za juu. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili.

5. Eleza maana ya istilahi zifuatazo, toa mfano kwa kila maana ya istilahi.

(a) Mawasiliano


(i) Maana...Ni..tendo....la...kupeana.....au...kupashana...habari..baina ya....watu...wawili....au...zaidi.

(ii) Mfano...Mwalimu....huweza....kuzungumza....na...mwanafunzi.....kuhusu...mitihani, tendo..hilo....la..kuzungumza...tayari..ni.......mawasiliano....baina...ya....watu.....wawili.

(b) Silabi

(i) Maana...Ni...muunganiko.....wa....konsonanti....na...irabu....au......irabu.....peke...yake....ambazo....hutamkwa....kama...fungu......moja....la.....sautina..hutumika..kuunda..maneno..mbalimbali.

(ii) Mfano...ba.,.cha..,.ka.,.de.,.ra.,.tu.,.na.,.a.,.i.
.......Ba.+.ba.=..Baba..,..Ki.+.cha.+.ka.=.Kichaka.


(c) Lugha

(i) Maana. Ni mfumo, mpangilio au utaratibu wa sauti za nasibu wenye kuleta maana na uliokubalika katika jamii ya watu ili uweze kutumika katika mawasiliano baina yao.

(ii) Mfano... Lugha ya Kiswahili inayotumika Tanzania, Lugha ya Kiingereza inayotumika katika nchi za Uingereza na Lugha ya Kifaransa inayotumika na Wafaransa huko Ufaransa.

(d) Irabu

(i) Maana... ni herufi zinazotamkwa bila kuzuizi chochote kinachozuia hewa kutoka kwenye mapafu, kupitia kinywani na kwenda nje.

(ii) Mfano... a, e, i, o, u.

(e) Sentensi

(i) Maana... Sentensi ni neno au mwungaiko wa maneno yaliyopangwa katika mpangilio maalum unaoleta maana.


(ii) Mfano... "Mama ameenda sokoni kununua nyanya," hii ni sentensi yenye maneno au idadi ya maneno matano (5).

Kielelezo Na. 5.1: *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 5.*

Katika Kielelezo Na. 5.1, mwanafunzi alieleza maana ya istilahi (a) hadi (e) na kutoa mifano inayowiana na maana hizo kwa usahihi.

Licha ya ufaulu mzuri wa wanafunzi katika kujibu swali hili, asilimia ndogo (9.4%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Kati yao, asilimia 1.3 walishindwa kueleza maana ya istilahi hata moja na kupata 0. Wanafunzi hao, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ndogo ya *Lugha kama Chombo cha Mawasiliano*, hivyo kushindwa kueleza maana na kutoa mifano stahiki ya istilahi hizo. Baadhi yao, walitungia sentensi istilahi walizopewa kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika tungo mchanganyiko kwa kutumia istilahi husika badala ya kueleza maana ya istilahi hizo ambapo aliandika katika (a) *Mawasiliano kati ya nchi na nchi ni muhimu sana*, (b) *Silabi huru ni nzuri zaidi*, (c) *Lugha ya Kiingereza ni ngumu*, (d) *Irabu haiwezi kutumika kwenye lugha* na (e) *Sentensi hazina maana*. Kwa ujumla, wanafunzi hao walitakiwa kueleza maana za istilahi kama

ifuatavyo: (a) *Mawasiliano* ni hali ya kutoa na kupokea habari/kupeana habari baina ya watu wawili au zaidi. (b) *Silabi* ni sehemu ya neno inayoundwa na konsonanti na irabu. (c) *Lugha* ni sauti za nasibu za kusemwa/kutamkwa zenye kuleta maana zilizokubaliwa.... (d) *Irabu* ni herufi inayotamkwa kwa kusukuma nje hewa bila kuweka kikwazo/kizuizi na (e) *Sentensi* ni tungo inayojitosheleza kimaana ambayo kimsingi huhusisha tendo na mtendaji. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kueleza maana ya istilahi hata moja na kupata alama 0.





Kielelezo Na 5.2: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali 5.*

Katika Kielelezo Na. 5.2, mwanafunzi alishindwa kueleza maana na kutoa mfano kwa kila maana ya istilahi katika kipengele (a) hadi (e) badala yake katika kipengele (a) alinakili sehemu ya maelekezo ya swali hilo na katika kipengele (b) hadi (e) alinakili sentensi za swali la (4) na kutoa mifano isiyohusiana na istilahi alizopewa.

### 2.3.2 Swali la 6: Lugha ya Kimazungumzo

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali*, mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano* ambapo lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutumia lugha kwa ufasaha. Swali lilikuwa na vipengele vitano (a) hadi (e) vilivyomtaka mwanafunzi kutunga sentensi mbili kwa kutumia maneno yenye maana zaidi ya moja aliyopewa ili kutofautisha maana hizo. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10.

Wanafunzi 599,637 sawa na asilimia 99.7 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri kwani asilimia 73.2 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Wanafunzi kwa Asilimia katika Swali la 6.*

Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 60.6 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10, asilimia 12.6 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na asilimia 26.8 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Idadi kubwa ya wanafunzi (60.6%) walijibu vizuri swali hili kwa kuwa waliweza kubaini maana zaidi ya moja katika maneno mengi na kupata alama za juu. Miongoni mwao, asilimia 26.4 walipata alama zote (10) katika swali hili. Hawa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu utata katika maneno hivyo walibaini maana zaidi ya moja katika maneno waliyopewa kwa usahihi. Aidha, waliweza kutunga sentensi mbili kwa kila neno husika kwa kutofautisha maana zilizopo katika neno hilo. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vizuri swali hili kwa kutunga sentensi mbili kwa kila neno (a) hadi (e) na kutofautisha maana za neno husika.

6. **Maneno yafuatayo yana maana zaidi ya moja. Tunga sentensi mbili kwa kila neno ukitofautisha maana hizo.**

(a) Kaa

(i.) Daktari alikaa kwenye kiti cha thamani sana.

(ii) Mariam alivua kaa wengi sana baharini.

(b) Tai

(i) Baba hakupendelea kuvaa tai nyeusi na shati jeupe.

(ii) Mbuga ya mikumi inaongoza kwa kuwepo wa Tai wengi.

(c) Kata

(i) Mkamba alikata mti kwa ajili ya kutengeneza kuni.

(ii) Diwani aliwakilisha ujumbe serikalini kwa niaba ya kata ya mtoni.

(d) Kanga

(i) Dada alitoka nje pasipo kujifunika kanga kichwani.

(ii) Babu alikamata kanga na kumla porini.

(e) Ulezi

i) Nunua ulezi kwa ajili ya uji wa mtoto.


ii) Ulezi wake si wa kuonya watoto.

Kielelezo Na. 6: *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 6.*

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeweza kutunga kwa usahihi sentensi mbili kwa kila neno ili kutofautisha maana mbili za kila neno na kupata alama zote.

Hata hivyo, wanafunzi wachache (12.6%) walipata alama za wastani kutokana na kumudu kutunga sentensi sahihi kwa baadhi ya maneno na kushindwa kubainisha tofauti ya msingi inayodhihirika katika maana za baadhi ya maneno. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alipata alama za wastani kwa kutunga sentensi sahihi katika vipengele (a), (b) na (d) na kutunga sentensi zisizo sahihi katika vipengele (c) na (e) kwa kuandika; (c) *Kataa wito usikatae neno* na *Ukikaa bila kazi utajuta* na katika (e) akaandika; *ulezi sio ulevi* na *uliza ujibiwe* majibu yasiyokidhi maana za msingi za maneno aliyopewa ambapo katika (c) alitakiwa kuandika sentensi zenye maana ya 'kifaa cha kuchotea maji' na 'sehemu ya kijiji'. Hali kadhalika, katika kipengele (e) angeandika sentensi zinazomaanisha 'chakula kiitwacho ulezi' na 'malezi apewayo mtu/mtoto.'

Kwa upande mwingine, asilimia 26.8 ya wanafunzi waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango hafifu kutokana na kukosa maarifa ya kubaini maana mbili za maneno waliyopewa na kushindwa kutunga sentensi mbili ili kutofautisha maana zaidi ya moja zilizopo katika neno husika. Miongoni mwao, asilimia 20.8 walipata 0 kutokana na kushindwa kutunga sentensi hata moja kwa maneno waliyopewa. Baadhi yao, walifafanua maana zilizopo katika maneno waliyopewa bila kutunga sentensi na wengine walitunga sentensi zisizohusiana na maneno *kaa, tai, kata, kanga na ulezi* kama ilivyotakiwa. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya swali na kupata alama hafifu.


6. Maneno yafuatayo yana maana zaidi ya moja. Tunga sentensi mbili kwa kila neno ukitofautisha maana hizo.

(a) Kaa

i. Kaa aina ya mdudu anaye ishi kwenye maji.

ii. kukaa chini kwenye kiti.

(b) Tai

i. Tai aina ya ndege anaye ruka na hupenda kula mizoga.

ii. Tai aina ya vazi linalo valiwa shingoni.

(c) Kata

i. kata ni sehemu ndogo ya kijiji.

ii. kata yaani kukata kitu kama vile kukata nyanya kukata mboga n.k

(d) Kanga

i. kanga ni aina ya nguo ambayo huvaliwa na wana wake.

ii. kanga ni aina ya ndege anaye ishi porini.

(e) Ulezi

i. Ulizi ni kulea kitu au kukichunga kitu kama vile kulea mtoto n.k

ii. Ulezi ni aina ya nafaka ambazo hutumika kutengenezea uji

Kielelezo Na. 6.2*: Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 6.*

Katika Kielelezo Na. 6.2, mwanafunzi alishindwa kutunga sentensi mbili ili kutofautisha maana za neno husika kama swali lilivyomtaka badala yake alielezea maana zilizopo katika neno husika katika kipengele (a) hadi (e) kinyume na matakwa ya swali.

## 2.4 SEHEMU D: FASIHI KWA UJUMLA

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu ambayo yalimtaka mwanafunzi kukamilisha methali, kutegua vitendawili na kufafanua mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi.


### 2.4.1 Swali la 7: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususan mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukumbuka kauli mbalimbali za kifasihi.

Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na lilimtaka mwanafunzi kukamilisha methali zifuatazo:

(i) *Ukitaka kujua asili ya mwanga..............................*
(ii) *Ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma..................*
(iii) *Jina jema............................................................*
(iv) *Haraka haraka....................................................*
(v) *Mjukuu si mwana.................................................*

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 600,891 sawa na asilimia 99.9 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu. Swali hili lilijibiwa vibaya na wanafunzi wengi ambapo asilimia 7.2 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.





**Chati Na. 6***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 7.*

Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 92.8 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5, asilimia 7.0 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na asilimia 0.2 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10.

Asilimia 92.8 ya wanafunzi waliojibu swali hili walishindwa kukamilisha methali walizopewa na kupata alama hafifu. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, wanafunzi wengi waliojibu swali hili waliweza kukamilisha methali ya (iv) pekee iliyouliza; Haraka haraka - *haina baraka*. Wanafunzi wachache, sawa na asilimia 3.1 walipata 0 kutokana na kushindwa kubaini dhana halisi zilizojengwa katika

methali hivyo kushindwa kutambua miundo ya methali zote. Baadhi yao, walitoa kauli zinazopinga kauli zilizojengwa katika sehemu ya kwanza ya methali husika (kinyume) na wengine waliandika kauli/maneno yasiyofungamana na muundo wa methali husika japokuwa yalikuwa na uhusiano wa kawaida na yale yaliyotumika katika methali husika. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika maneno yanayoashiria kukamilisha sentensi zilizounda methali hizo badala ya kukamilisha methali husika. Mwanafunzi huyo aliandika majibu yafuatayo; (i) ....*washa taa,* (ii) ....*anaongea Kiingereza,* (iii) ......*hupewa na Mungu* (iv) ..... *hufika mapema* na (v) .....*huitwa mjukuu*; badala ya kukamilisha methali hizo kwa kuandika; (i) ...ingia gizani (ii) ....tazama tabu ya asiyesoma (iii) ......hung'aa gizani, (iv) .....haina baraka na (v) .....mrudishe kwao. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukamilisha methali alizopewa na kupata 0.


7. Kamilisha methali zifuatazo:

(i) Ukitaka kujua asili ya mwanga… ujue unapotea.

(ii) Ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma… Kutembea Kwake

(iii) Jina jema… barabara


(iv) Haraka haraka… aina chochote

(v) Mjukuu si mwana… Anisaidii chochote

Kielelezo Na. 7.1: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 7.*

Katika Kielelezo Na. 7.1, mwanafunzi aliandika maneno/vifungu vya maneno vinavyoashiria kukamilisha sentensi zilizoundwa katika sehemu ya kwanza ya methali (i) hadi (v) kinyume cha matakwa ya swali badala ya kukamilisha methali hizo kama ilivyotarajiwa.

Wanafunzi wachache sawa na asilimia 7.0 walipata alama za wastani. Wanafunzi hao, walionesha kuwa na uelewa wa baadhi ya methali hivyo kuweza kujibu baadhi ya methali walizopewa. Wengi wao waliweza kukamilisha methali tatu tu kwa usahihi na kushindwa mbili hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kukamilisha baadhi ya methali na kupata alama za wastani.



7. Kamilisha methali zifuatazo:

(i) Ukitaka kujua asili ya mwanga.....ingia.....gizani...........................

(ii) Ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma......mafanikio.....yake..............

(iii) Jina jema......hung'ara.....gizani..................................................

(iv) Haraka haraka...haina.....baraka..................................................

(v) Mjukuu si mwana......bali.....mpita....njia:.......................................

Kielelezo Na. 7.2: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi lisilojitosheleza katika swali la 7.*

Katika Kielelezo Na. 7.2, mwanafunzi aliweza kukamilisha methali tatu katika kipengele cha (i), (iii) na (iv) kwa usahihi na kushindwa kukamilisha methali mbili kwa kuandika; (ii) "mafanikio yake" badala ya *tazama taabu ya asiyesoma* na (v) "bali mpita njia" badala ya *mrudishe kwao* kama ilivyotakiwa.

Wanafunzi wachache sana ambao ni sawa na asilimia 0.2 pekee ndio walioweza kukamilisha methali katika vipengele vingi na kupata alama za juu kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu muundo wa methali unaotokana na pande mbili za kauli zinazotegemeana. Hivyo, wanafunzi hao waliweza kukamilisha methali walizopewa kwa kuwa walihusisha pia na semi/kauli mbalimbali zinazotumika katika mazingira yao hivyo kuandika kwa usahihi katika kipengele (i) ...ingia gizani (ii) ....tazama tabu ya asiyesoma (iii) ......hung’aa gizani, (iv) .....haina baraka na (v) .....mrudishe kwao.

### 2.4.2 Swali la 8: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususan mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi* ambapo lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuelewa mafumbo yaliyojengwa katika vitendawili. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na lilimtaka mwanafunzi kutegua vitendawili vifuatavyo:

*(i) Gari langu halitumii mafuta*..............................


*(ii) Napigwa faini kosa silijui*.........................................

*(iii) Kamba yangu ndefu lakini haifungi kuni* ..................................

*(iv) Ukiona njigi utadhani njege na ukiona njege utadhani njigi* .......

*(v) Nyumba yangu ndogo wapangaji wengi* ......................................


Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 600,942 sawa na asilimia 99.9 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri zaidi cha ufaulu kwani asilimia 96.5 walipata alama za wastani hadi za juu. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 8.*

Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 56.3 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10, asilimia 40.3 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na asilimia 3.4 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5.

Asilimia 56.3 ya wanafunzi walijibu vizuri swali hili kwani walikuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu tungo za kifasihi na kuweza kufumbua mafumbo yaliyotegwa katika vitendawili walivyopewa. Aidha, vitendawili vyote walivyopewa ni vile vilivyozoeleka kutumika katika mazingira ya kawaida hivyo kuwawezesha wanafunzi wengi kuvitegua kwa usahihi. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kutegua vitendawili vyote na kupata alama zote 10.



8. Tegua vitendawili vifuatavyo:

(i) Gari langu halitumii mafuta…Miguu…

(ii) Napigwa faini kosa silijui …Kujikwaa…

(iii) Kamba yangu ndefu lakini haifungi kuni …Njia…

(iv) Ukiona njigi utadhani njege na ukiona njege utadhani njigi…Maziwa na tui la nazi


(v) Nyumba yangu ndogo wapangaji wengi …Kiberiti…

Kielelezo Na. 8.1: *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 8.*

Katika Kielelezo Na. 8.1, mwanafunzi alitegua vitendawili kwa usahihi katika vipengele (i) hadi (v) kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha ya kufumbua mafumbo yaliyojengeka katika vitendawili hivyo pamoja na kuzingatia matakwa ya swali.

Hali kadhalika, asilimia 40.3 ya wanafunzi waliojibu swali hili waliweza kutegua baadhi ya vitendawili na kushindwa vingine, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitegua vitendawili (i), (iv) na (v) kwa usahihi na kushindwa (ii) na (iii) kwa kuandika (ii) *polisi* na (iii) *nyoka* badala ya *kujikwaa* na *njia* mtawalia. Majibu yasiyo sahihi ya mwafunzi huyo yalitokana na kushindwa kufumbua mafumbo yaliyojengeka katika vitendawili hivyo hatimaye kuandika maneno ya moja kwa moja yanayoelekea kufanana na kauli zilizokuwa katika vitendawili hivyo.

Licha ya ufaulu mzuri wa wanafunzi katika swali hili, wanafunzi wachache sana sawa na silimia 3.4 walishindwa kujibu kwa usahihi na kupata alama hafifu. Wanafunzi hao, walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mafumbo yaliyojengwa katika vitendawili hivyo, kushindwa kutegua vitendawili walivyopewa. Baadhi yao, waliandika maneno ya moja kwa moja yanayoelekea kufanana na kauli zilizokuwa katika vitendawili hivyo badala ya kufumbua mafumbo yaliyojengwa katika vitendawili husika. Kwa mfano mwanafunzi mmoja alitoa majibu yafuatayo; (i)...*farasi* (ii)....*maandazi* (iii)....*kamasi* (iv)....*kioo* na (v).....*nanasi* badala ya ...miguu, ...kujikwaa, ....njia, ....maziwa na tui la nazi na ....kiberiti mtawalia. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kabisa kutegua kitendawili hata kimoja na kupata alama hafifu.



8. Tegua vitendawili vifuatavyo:

(i) Gari langu halitumii mafuta…Baiskeli……………………………………

(ii) Napigwa faini kosa silijui …Fimbo……………………………………

(iii) Kamba yangu ndefu lakini haifungi kuni …Mkanda……………………………

(iv) Ukiona njigi utadhani njege na ukiona njege utadhani njigi…Uso……………

(v) Nyumba yangu ndogo wapangaji wengi …Mayai………………………………


Kielelezo Na. 8.2: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 8.*

Katika Kielelezo Na. 8.2, mwanafunzi aliandika majibu yasiyo sahihi ya vitendawili katika kipengele cha (i) hadi (v) na yasiyozingatia uhalisia wa vitu na mazingira yaliyotumika kuunda vitendawili husika, hivyo kushindwa kutegua vitendawili vyote na kupata 0.

### 2.4.3 Swali la 9: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji wa Kazi za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuunda katika kutunga kazi za kifasihi. Swali lilimtaka mwanafunzi kufafanua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi na lilikuwa na jumla ya alama 10.


Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 586,968 sawa na asilimia 97.6 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya kwani asilimia 31.6 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 8***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 9.*

Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 68.4 walikuwa na kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5, asilimia 27.4 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na asilimia 4.2 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10.

Idadi kubwa, (68.4%) ya wanafunzi walijibu swali hili vibaya na kufaulu kwa kiwango hafifu. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, baadhi ya watahiniwa waliweza walibaini jambo moja muhimu katika utunzi wa hadithi na wengine sawa na asilimia 35.3 walipata 0 kutokana na kukosa maarifa na ujuzi wa kutunga hadithi hivyo kushindwa kufafanua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi. Baadhi yao, walitunga hadithi mbalimbali na kutaja/kuelezea aina za hadithi na wengine walifafanua dhima za fasihi simulizi kinyume cha matakwa ya swali badala ya kufafanua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi kama vile; *mwanzo na mwisho wa hadithi*, *lugha ya kimasimulizi/ kimaelezo, aina ya wahusika kama vile watu, wanyama na vitu, dhamira kuu/lengo kuu/ tukio kuu* na *mandhari ya hadithi*. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kufafanua mambo muhimu katika kutunga hadithi na kupata alama hafifu.


9. Fafanua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi.

(a) Tarihi
Nihadithi zinazo simulia mambo ya kihistoria.

(b) Mekaya

(c) Soga
Nihadithi ambazo hubuniwa na watu.

(d) ngano

(e) vigano

Kielelezo Na. 9.1: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 9.*

Katika Kielelezo Na. 9.1, mwanafunzi alishindwa kufafanua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi badala yake alitaja aina za hadithi na kueleza maana kwa baadhi ya aina hizo kinyume na matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, asilimia 27.4 ya wanafunzi walioweza kujibu swali hili waliweza kufafanua baadhi ya mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi na kushindwa kufafanua mambo mengine hivyo kufaulu kwa kiwango cha wastani. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alifafanua kwa usahihi hoja tatu zinazohusu mandhari, matumizi ya lugha ya masimulizi  na wahusika lakini katika hoja mbili nyingine alifafanua hoja sisizo sahihi kama *kuwasilishwa kwa mdomo* na *hurithishwa kizazi hadi kizazi* badala ya kuelezea mwanzo/mwisho wa hadithi na  dhamira/lengo la hadithi, hivyo kupata alama za wastani.

Wanafunzi wachache sana sawa na asilimia 4.2 walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu. Wanafunzi hao, walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi. Hivyo, walimudu kufafanua mambo hayo kama vile; *mwanzo*

*na mwisho wa hadithi wa kuvutia, lugha ya kimasimulizi/ kimaelezo, aina ya wahusika, dhamira kuu/lengo kuu/ tukio kuu* na *mandhari ya hadithi*. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliweza kufafanua kwa usahihi mambo hayo kama inavyodhihirishwa katika Kielelezo Na. 9.2.

9. Fafanua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi.

(a) Hadithi inayotungwa ni lazima izingatia matumizi ya lugha fasaha na inayoeleweka, pia ihakikishe kuwa lugha inayotumika iwe inayofuata taratibu zote za kisarufi pia izingatie kuwa matumizi yake yakidhi vigezo vyote vya mila na desturi na tamaduni za lugha hiyo.

(b) Hadithi inayotungwa ni lazima iwe na wahusika watakobeba waisifu fulani katika hadithi, pia matumizi ya majina ya wahusika kama wanyama yaendane na tabia zao halisi Mfano: Sungura - ujanja, Fisi - tamaa na uchu wa kitu fulani, Simba - Kiongozi wa jamii ama eneo fulani.

(c) Hadithi hiyo ilenge au ihakikishe kuwa ujumbe uliokusudiwa utafika kwa watu husika pia ujumbe kusudiwa usifichwe sana ili kila mtu atakayesikia au kusoma aweze kuuelewe ujumbe kwa uharaka na kwa uharaka zaidi.

(d) Hadithi hiyo pia izingatie mtiririko mzuri wa visa na matukio Mfano: Mtunzi anaweza kutumia muundo wa mbele na nyuma, muundo wa mbele tu, na muundo rejeshi ila azingatie visa hivyo visigongane gongane vyote vieleze jambo husika.

(e) Pia mtunzi aweze kuzingatia mandhari au eneo ambapo hadithi hiyo au kisa hicho kilipofanyika Mfano: Porini, Misituni, Nchi au eneo fulani. pia mandhari iendane na kisa husika yaani kuwa na uwiano baina ya mandari na kisa pamoja na wahusika

Kielelezo Na. 9.2: *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 9.*

Katika Kielelezo Na. 9.2, mwanafunzi aliweza kufafanua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutunga hadithi katika vipengele (a) hadi (e) kwa usahihi kwa kufafanua *matumizi ya lugha fasaha*, *wahusika*, *ujumbe uliokusudiwa*, *mtiririko mzuri wa visa na matukio* na *mandhari au eneo la hadithi* na kupata alama zote 10.

## 2.5 SEHEMU E: UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lililomtaka mwanafunzi kuandika simu ya maandishi kwa maneno yasiyozidi kumi (10).

### 2.5.1 Swali la 10: Uandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi*, mada ndogo ya *Simu ya maandishi* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuunda dhana/mawazo mbalimbali ya habari/nathari ili kufikisha ujumbe fulani. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15 na lilimtaka mwanafunzi kuandika simu ya maandishi ili kumjulisha dada yake kuwa mama yao ni mgonjwa.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 595,370 sawa na asilimia 99.0 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji. Ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri ambapo asilimia 75.2 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.

**Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi**

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 - 4.0 | 147,652 | 24.8 |
| 4.5 - 9.5 | 102,404 | 17.2 |
| 10 - 15 | 345,314 | 58.0 |

Zaidi ya nusu ya wanafunzi (345,314) sawa na asilimia 58.0 walifaulu kwa kiwango kizuri. Ufaulu mzuri wa wanafunzi katika swali hili umetokana na maarifa ya kutosha waliyo nayo kuhusu uandishi wa simu ya maandishi. Wanafunzi hao, waliandika simu kwa kuzingatia *anwani ya mwandikiwa, ujumbe uliokusudiwa kwa mlengwa, jina la mwandishi au mtuma simu, kuandika maneno yote kwa herufi kubwa*

*na kuzingatia idadi ya maneno.* Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeandika kwa usahihi simu ya maandishi kwa kuzingatia taratibu zote za uandishi na kupata alama zote 15.

10. Kwa maneno yasiyozidi kumi (10) mtumie simu ya maandishi dada yako Lulu Mwendokasi wa S.L.P 1012 Mwanza, kumfahamisha kuwa, mama yenu anaumwa. Jina lako liwe Mwasi Mwendokasi.


LULU MWENDOKASI SLP 1012 MWANZA DADA
MAMA ANAUMWA MWASI MWENDOKASI.

Kielelezo Na.10: *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 10.*

Katika Kielelezo Na. 10.1, mwanafunzi aliweza kuandika simu ya maandishi iliyozingatia vigezo vyote stahiki na kupata alama za juu.

Hata hivyo, wanafunzi wachache (102,404) sawa na asilimia 17.2 walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kuandika simu iliyozingatia baadhi ya vigezo vya uandishi huo kama vile idadi stahiki ya maneno na mpangilio sahihi wa simu ya maandishi, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika simu yenye ujumbe sahihi lakini alianza na jina la mwandishi *MWASI MWENDOKASI* badala ya LULU MWENDOKASI ambaye ndiye aliyekuwa anaandikiwa simu husika, hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi (147,652) sawa na asilimia 24.8 walipata alama hafifu kutokana na kukosa maarifa na uelewa kuhusu simu ya maandishi. Baadhi yao, waliandika simu ya maandishi isiyozingatia baadhi ya vigezo kama vile; anwani ya mwandikiwa kuwekwa mwishoni au katikati, ujumbe usio kamili, kutokuandika jina la mwandishi au mtuma simu, kuandika maneno ya simu kwa herufi ndogo na kutozingatia idadi ya maneno, hivyo kupata alama hafifu. Wanafunzi wengine waliandika barua za kirafiki na za kikazi kinyume cha matakwa ya swali na kupata 0. Kielelezo Na.10.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika barua badala ya simu na kupata alama hafifu.



10. Kwa maneno yasiyozidi kumi (10) mtumie simu ya maandishi dada yako Lulu Mwendokasi wa S.L.P 1012 Mwanza, kumfahamisha kuwa, mama yenu anaumwa. Jina lako liwe Mwasi Mwendokasi.

Lulu MWENDOKASI,
S.L.P 1012,
mpenda dada Mwanza,
ni mimi mdogo wako ninataka kakujilisha
kwamba mama anaumwa
ni mimi mwasi mwendokasi.

Kielelezo Na.10.2: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 10.*

Katika Kielelezo Na. 10.2, mwanafunzi alishindwa kuandika simu ya maandishi kama ilivyotakiwa badala yake aliandika barua ya kirafiki iliyokuwa na makosa ya kitahajia na ya kimuundo, hivyo kupata alama 0.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili unaonesha kuwa, mada tatu kati ya tano zilizopimwa mwaka 2020 yaani *Ufahamu, Mawasiliano na Matumizi ya Lugha*, pamoja na *Uandishi wa Insha/Utungaji* zilikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 89.0, 81.9 na 75.2 mtawalia. Aidha, mada mbili zilikuwa na ufaulu wa wastani yaani *Sarufi* (62.3%) na Fasihi (45.1%). Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa katika upimaji huu, zipo mada zilizoonesha kuongezeka na nyingine kushuka kwa kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Mada tatu zilizokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa mwaka 2020 zilionesha kuongezeka kiwango cha ufaulu ikilinganishwa na mwaka 2019. Mada hizo ni *Ufahamu* uliokuwa na nyongeza ya asilimia 4.5 kutoka (84.5%) hadi (89.0%), *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha* kutoka (62.2%) hadi (81.9%) ikiwa na ongezeko la (19.7%) na *Uandishi wa Insha/Utungaji* kutoka (54.7%) hadi (75.2%) kwa ongezeko la asilimia 20.5. Hivyo, uchambuzi huu unaonesha kuwa, ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi umeendelea kuimarika siku hadi siku.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, mada mbili zilizokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu katika upimaji huu, ufaulu wake ulishuka. Mada hizo ni *Sarufi* iliyopungua kidogo kutoka 63.1% hadi 62.3% ikiwa na upungufu wa asilimia 0.8 na *Fasihi* ambayo ufaulu wake umepungua kwa kiasi kikubwa cha asilimia 17.8 kutoka (62.9%) hadi (45.1%).

Wastani wa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika mada zote kwa mwaka 2020 ni asilimia 70.7, kiwango ambacho ni cha juu kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo wastani wa kiwango cha ufaulu kwa mada kilikuwa 65.5%. Hivyo, kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2020 kimeongezeka kwa kuwa wanafunzi wengi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizopimwa na hivyo kutoa majibu yaliyojitotesheleza kwa maswali mengi.

Kwa jumla, mada iliyokuwa na wastani wa chini zaidi wa ufaulu kwa mwaka 2020 ni mada ya *Fasihi* kutokana na wanafunzi wengi kukosa maarifa na ujuzi wa kutosha katika kukamilisha methali. Hata hivyo, mada hii, pamoja na mada ya *Sarufi* zilizokuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani zinatakiwa kutiliwa mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea wanafunzi msingi mzuri wa maarifa na kuwafanya kuwa mahiri katika somo la Kiswahili. Ufaulu wa wanafunzi katika mada mbalimbali kwa mwaka 2020 umeainishwa katika **Kiambatisho A**. Pia, ulinganifu wa viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika mada kwa mwaka 2019 na 2020 umeainishwa katika **Kiambatisho B.**

## 4.0 HITIMISHO

Upimaji wa Kidato cha Pili kwa mwaka 2020 katika somo la Kiswahili ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalipimwa kwa kuzingatia majazi ya utambuzi ambayo ni *kuelewa, kukumbuka, kutumia, kuchambua, kutathmini* na *kuunda*. Ufaulu wa wanafunzi kwa ujumla ulikuwa mzuri ambapo asilimia 92.38 walifalu katika upimaji huu.

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali kama vile, wanafunzi wengi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizopimwa hususan *Sarufi na Fasihi*. Aidha, baadhi ya wanafunzi walionesha kutokuzingatia matakwa ya maswali ipasavyo hivyo kushindwa kujibu maswali waliyopewa.

Hata hivyo, uchambuzi huu unaonesha kuwa, zipo mada zinazohitaji jitihada za dhati katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii ni kwa sababu ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka 2020 katika mada za *Fasihi* (45.1%) na *Sarufi* (62.3%) zimeendelea kuwa na ufaulu wa wastani tangu mwaka 2019. Aidha, mada ya *Fasihi* (45.1%) imekuwa na ufaulu wa chini zaidi kwa mwaka 2020 kwa upungufu wa asilimia 17.8 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Mwisho, taarifa hii ya upimaji kuhusu uchambuzi wa majibu ya wanafunzi wa Kidato cha Pili ikitumika ipasavyo itakuwa chachu na dira ya mabadiliko kutoka ufaulu wa wastani hadi ufaulu mzuri katika mada mbalimbali za somo la Kiswahili. Hata hivyo, hii ni mojawapo ya utatuzi wa changamoto kwa walimu na wanafunzi katika swala zima la ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Aidha, uchambuzi huu utawawezesha kuelewa makosa mbalimbali yanayosababisha kushuka kwa ufaulu kwa baadhi ya mada ili kuwa na ufaulu wa juu wakati mwingine.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili hususan kwa mada zilizokuwa na kiwango cha wastani, inashauriwa:

(a) Wanafunzi wapewe mazoezi ya kutosha ili waweze kupata umahiri na maarifa ya kutosha katika mada za *Sarufi* na *Fasihi*.

(b) Kutumia vielelezo vya kufundishia vinavyoakisi miundo na matumizi ya vitendawili na kauli za vitenzi.

(c) Kuongoza wanafunzi katika kufanya utafiti/kazi mradi ili kubaini mbinu mbalimbali za kifani zilizotumika katika utunzi wa kazi za kifasihi hususan hadithi.

(d) Mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile midahalo, na maigizo kwenye vikundi vidogo vidogo zitumiwe na walimu ili kuwaongezea wanafunzi ujuzi na maarifa katika mada ya *Sarufi* na *Fasihi* zilizokuwa na ufaulu wa chini.

(e) Walimu watumie njia ya majadiliano na vielelezo vya kufundishia (zana za kufundishia) zinazopatikana katika mazingira halisi. Aidha, mada zote zifundishwe kwa vitendo ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi kwa kulinganisha anachofundishwa na uhalisia wake.

**KIAMBATISHO A**

## UCHAMBUZI WA VIWANGO VYA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2020

| Na. | Mada | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Na. ya Swali | % ya Ufaulu (alama $30^{+}$) | | |
| 1. | *Ufahamu* | 1 | 91.3 | 89.0 | Vizuri |
| | | 2 | 86.6 | | |
| 2. | *Mawasiliano na Matumizi ya lugha* | 5 | 90.6 | 81.9 | Vizuri |
| | | 6 | 73.2 | | |
| 3. | *Uandishi wa Insha/Utungaji* | 10 | 75.2 | 75.2 | Vizuri |
| 4. | *Sarufi* | 3 | 53.3 | 62.3 | Wastani |
| | | 4 | 71.3 | | |
| 5. | *Fasihi kwa Ujumla.* | 7 | 7.2 | 45.1 | Wastani |
| | | 8 | 96.5 | | |
| | | 9 | 31.6 | | |

**KIAMBATISHO B**

**ULINGANIFU WA VIWANGO VYA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2019/2020**

